


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA SABA

03 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI NA SABA – TAREHE 03 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

212. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali italigawa Jimbo la Kilindi.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

213. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED ABDALLAH (LINDI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaipatia fedha Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ili iweze kutekeleza mradi wa kimkakati wa ujenzi wa Soko Kuu.

214. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Shule za Sekondari za Lyamahoro na Rubale zitaanza kutoa elimu ya Kidato cha Tano na Sita.

215. MHESHIMIWA JOSEPH KASHEKU MUSUKUMA (GEITA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa Hosteli katika Shule ya Sekondari ya Rubanga ili iwe ya Kidato cha Tano na Sita.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

216. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMED ISSA (MTAMBWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, ni kero gani za Muungano zilizoibuliwa na kutatuliwa toka kuasiwiwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

217. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Vituo vya Abiria vya Bugorola, Ukara na Kisorya Ukerewe.

218. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali imetoa Mwongozo gani kuhusiana na kiwango cha ubora wa taa zinazowekwa Barabarani.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

219. MHESHIMIWA OMAR ALI OMAR (WETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka magari kwa Jeshi la Polisi - Mkoa wa Kaskazini Pemba.

220. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH (DONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza ajali zinazosababishwa na magari ya mchanga Wilaya ya Kaskazini B - Unguja.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

221. MHESHIMIWA NJALU DAUDI SILANGA (ITILIMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mahakama ya Ardhi chini ya Mhimili wa Mahakama.

WIZARA YA KILIMO:

222. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kushusha bei ya mbolea na pembejeo nyingine za kilimo ili kuongeza uzalishaji.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

223. MHESHIMIWA HAJI MAKAME MLENGE (CHWAKA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itawalipa fedha zao waathirika wa Benki ya FBME iliyofilisiwa tangu Mei 2017.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

224. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa nini Serikali isiagize kuwe na Madereva na Kondakta wa jinsia zote kwenye Mabasi ya Shule ili kudhibiti vitendo vya ubakaji.

WIZARA YA MAJI:

225. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE RWAMLAZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itapeleka maji Kata za Maruku, Karabagaine, Nyakato, Kunazi, Katoma, Kemondo na Bujugo jirani na Bukoba Manispaa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
03 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, ndc
KATIBU WA BUNGE**